

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO




TAREHE 15/ 3/2018

TANGAZO LA ZABUNI YA UKAMILISHAJI UJENZI WA BWENI SHULE YA SEKONDARI ZAKIA MEGHJI

ZABUNI NA: 02

1. Bodi ya shule ya sekondari ZAKIA MEGHJI imepokea fedha za P4R Kutoka OFISI YA RAIS-TAMISEMI kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule.
2. Mwenyekiti bodi ya shule ya sekondari Zakia Meghji wilaya ya Chato anakaribisha maombi kutoka kwa wamiliki wa magari / wauzaji wa mchanga ndani ya Halmashauri ya wilaya ya Chato.
3. Mwombaji ambaye ni mmiliki wa gari/ magari atatakiwa kutuma maombi ya kuwa mzabuni kwa kuanisha aina ya gari, namba ya usajili, uwezo wa gari (capacity), na idadi ya magari anayomiliki ambayo anatarajia kuyatumia.
4. Mwombaji atapaswa kutaja kiasi cha malipo, mathalani tripu 1 ni sawa na shilingi ngapi kwa kuanisha mchanganuo ufuatao.
 - Trip moja ni Tsh Endapo mchanga ni wa mzabuni na kwamba vifaa tajwa atavisafirisha kutoka wapi (mfano kutoka chato bwangan.k) hadi eneo la ujenzi.
 - Trip moja Tsh. ikiwa mchanga utatolewa na bodi ya shule, mzabuni kazi yake ni kusomba kutoka..... na kuhakikisha mchanga umefikishwa eneo husika la ujenzi.
5. Mwombaji athibitisha kuwa gari lake litafanya kazi muda wote wa mkataba.
6. Katika maombi yake mwombaji atatakiwa kuambatanisha nakala ya hati ya umiliki wa gari / magari na tin namba. Aidha, jina la mwombaji lazima lifanane katika kumbukumbu zote za umiliki wa gari na ndilo litakalo tumika wakati wa kuandaa na kufanya malipo husika.
7. Mwombaji wa uzabuni wa kuuza mchanga atapaswa kutaja kiasi cha malipo mfano trip moja ni shilingi ngapi kwa kuanisha aina ya gari, namba ya usajili na uwezo wa gari.

8. Maombi ya zabuni yaandikwe kwa herufi kubwa yakionyesha namba ya zabuni na jina la zabuni inayohusika na yawekwe kwenye bahasha isiyo na mchoro au maandishi yafungwe vizuri na yatumwe kwa:
**KATIBU (MKUU WA SHULE),
SHULE YA SEKONDARI ZAKIA MEGHJI
S L P 210 CHATO.**
9. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **21/3/2018** saa nne asubuhi. Zabuni zitafunguliwa siku hiyo mara baada ya muda wa kupokea zabuni kuisha katika ofisi ya mkuu wa shule au mahali popote kutakapokuwa kumeandaliwa.



**KATIBU BODI YA SHULE
SHULE YA SEKONDARI ZAKIA MEGHJI**

Katibu Mkuu wa Shule
SHULE YA SEKONDARI ZAKIA MEGHJI
S.L.P 210
CHATO